

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Simu: +46 8 732 24 30/31
Fax: +46 8 732 24 32
Email: mailbox@tanemb.se
Web: www.tanemb.se

Ubalozi wa Tanzania
Näsby Allé 6
183 55 Täby
Stockholm
Sweden

Kumb. Na: NA.38/605/01

23 Julai, 2018

KONGAMANO LA TANO LA DIASPORA (FIFTH DIASPORA CONFERENCE) LITAKALOFANYIKA ZANZIBAR, TAREHE 18-19 AGOSTI 2018.

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.


Ubalozi unapenda kuwafahamisha kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, imeandaa kongamano la Tano la Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) litakalofanyika tarehe 18-19 Agosti 2018 katika Hoteli ya Verde iliyopo Mtoni, Zanzibar.

Kongamano hilo linakadiriwa kuwa na washiriki zaidi ya 300 wakiwemo Diaspora, Ex- Diaspora na wadau mbalimbali wa Maendeleo kutoka sekta Binafsi. Washiriki watapata fursa ya kubadilishana mawazo juu ya mbinu na mikakati ya kuimarisha mazingira yatakayowawezesha Diaspora kuongeza kasi ya ushiriki wao katika kuleta maendeleo chanya ya Taifa kupitia fursa za uwekezaji, Biashara na Utalii.

Kauli mbiu ya Kongamano ni **DIASPORA NA MAENDELEO**, ikienda sambamba na motto ya "*Mtu kwao ndio Ngao*".

Pamoja na barua hii, tunaomba taarifa hii ifikishwe kwa Diaspora wote na kuwahamasisha ili wafanye maandalizi ya kwenda nchini kushiriki Kongamano hili muhimu. Taarifa zingine muhimu ikiwemo ratiba nzima ya Kongamano hilo zitawasilishwa hapo baadae.

Tunatanguliza shukrani za dhati kwa ushirikiano wen una tunawatakia kazi njema.


Matiku Kimenya
Kny: BALOZI